Khawarij na Murji'ah

Hawana Tofauti

Sh. Abdul Malik Ahmad ibn al-Mubaarak ar-Ramadaani

Asli: Madaariku an-Nadhr (na nyongeza)

Imefasiriwa na: Abu Farida Muhammad Basawwad

بسم الله الرحمن الرحيم

Sababu zilizonipelekea mimi kuingiza mlango huu (kwenye kitabu) ni kwamba nimewapeleleza wengi wa hawa (wafuasi wa mapote) washupavu wakiwashutumu mashekhe wetu wa Sunnah, Sheikh Ibn Baaz, Sheikh Al-Albaani, na Sheikh Ibn 'Uthaymeen yakuwa wao ni Murji'ah. Sababu ya shutuma hizi ni kwamba mashekhe hawa wameifafanua maana ya ayah hii **'na yoyote asiyehukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu…'** kwa uwazi kama inavyostahiki na ifahamikavyo kutoka kwa Salaf., na pia kwa sababu wao hawakufurishi mtu bila ya kupatikana masharti kamili [1]. Na vievile, hawa mashekhe wanakataza kumu'asi kiongozi dhalimu miongoni mwa Waislamu. Na hata kama imewadhihirikia wao ukafiri wa dhahir, wao wataendelea kukataza ikiwa hawatokuwa na uwezo wa kufanya hayo na wala hakuna faida yoyote ya ki-Sheriya itakayopatikana.

Kwahivyo mimi nasema,

La Kwanza: Matamshi au hukmu ya kujitokeza wazi katika mapinduzi dhidi ya viongozi, kwa uhakika ni madh-hab (mifumo) ya Murji'ah, kwani Ibn Shahin amepokea kutoka kwa [Sufyaan] ath-Thawree yakwamba amesema, "Inajuzu kulingana na msimamo wa Murji'ah kutumia upanga dhidi ya watu wa Qiblah (Waislamu kwa ujumla)." [2]

Vilevile akapokea yakwamba aliulizwa Ibn al-Mubaarak, "Wewe una msimamo wa Irjaa'?" Nae akajibu, "Nitakuwaje Murji' ikiwa msimamo wangu ni kwamba si halali kujitokeza na upanga (dhidi ya Waislamu)." [3]

Zaidi ya hayo, as-Saabuni (k. 449) akapokea kwa upokezi ulio saheeh mpaka kwa Ahmad bin Sa'id ar-Ribati yakwamba amesema, "Nimeambiwa na *'Abdullah bin Tahir* , 'Ewe Ahmad, amma kwa hakika chuki zenu juu ya hawa (yaani Murji'ah) imeegemezwa juu ya ujinga, na mimi ninawachukia (hawa Murji'ah) juu ya 'Ilmu. Kwanza, hawaamini yakwamba inawapasa kuwa watiifu kwa kiongozi…" [4]

Mimi nasema: Kwani maandishi haya hayatoshi kuwa ni dalili yakwamba wao (yaani Safar al-Hawali, Salma al-Awdah, na 'Ali bin Haj, na kadhaalika) ndiwo Murji'ah wa kihakika na kwamba Wanavyuoni wetu tuliowataja hapo awali hawahusiki na hayo!

Uchunguzi muhimu: Jambo la kushangaza ni kwamba Safar al-Hawali ameshindwa kuyafahamu haya mafungamano yaliyo dhahiri baina ya Murji'ah na Khawaarij. Alisema, "Kama ilivyopokewa kutoka kwa Imaam Ahmad matamshi yenye maana magumu kuyafahamu nayo ni kwamba: 'Kwa hakika Khawaarij, ndiwo Murji'ah'"! Kisha baada ya hapo akaja na mlipuko usioweza kuvumilika, akasema, **"Kuna uwezekano wa ufafanuzi wa maneno haya kuhusu Irja' ya maswahaba"!!! [5]**

Mimi nasema: Lau kama angeliziendeleza riwaya zilizopita basi angelijuwa yakwamba si jambo gumu kuyafahamu mafungamano baina ya Murji'ah na Khawaarij katika ku'asi dhidi ya viongozi.

Na wala isiwe ni jambo la kustaajabisha kuhusu jambo hilo yakwamba Irja' itajitokeza na kusambaa muda mchache baada ya ku'asi (kufanya mapinduzi). Akasema Qatadah, "[Uzushi wa] Irja' ilijitokeza baada ya mkasa wa *Ibn al-'Ash'at* (mmojawapo wa watetezi wa Khawaarij) [6]

Katika ushahidi mwengine wenye kuonyesha yakwamba watu hawa wapo juu ya (Imani ya Uzushi ya) Irja' ni kama ufuatao:

La Pili: Ni kwamba wao hawataraji kuhusu nafsi zao yakwamba wana imani zilizokamilika na chochote chenye kuandama kutokea hapo – hata kama mmoja wao atasema waziwazi yakuwa anaandama njia ya Salaf. Kwani wewe huoni wakisema, "Hassan al-Bannah Shahid…" na "Shahid Sayyid Qutb"? Na mmojawapo anapoambiwa, "Iwapo kuwasifu wao kuwa ni ma-Shahid ni jambo la waajib katika pote lao, jambo wasiloweza kuliepuka kutamka, basi angalau kwa uchache waongeze 'Insha-Allaah (Akipenda Allaah).'"

Imaam al-Bukhaari ametia kwenye mlango wa kitabu cha Jihaad katika Saheeh yake akasema, "Mlango: Haifai kusema yakwamba fulani na Fulani ni Shahid", na akataja dalili zake chungu nzima. Na hili ni jambo lililosisitizwa kutoka kwao mara kwa mara, lakini wao wakawa ni watu wenye viburi na madharau, wakisema badala yake, "Nyinyi munaidunisha (kuifanya duni) Jihaad na kuzifanyia mzaha habari na taarifa zinazohusiana na mas-ala ya kilimwengu!!"

Mimi nasema pia kuhusu ukanushaji huu wa kujifanyia mtu mwenyewe (au wengine kutokamana na walio na imani iliyokamilika au kutokamana na waliohakikishiwa kuingia peponi, n.k). Yakwamba 'Abdur-Rahman bin Mahdi – Rehma za Mwenyezi Mungu zimshukie – amesema, "Misingi ya irja' ni kuipinga kwa nafsi yake (au wengine kwa kutokuwa na Imani iliyokamilika au kutohakikishiwa kuipata pepo, n.k)". [7]

La Tatu: Tukirudi kwenye mjadala wetu wa asli (katika kitabu hiki), mimi nasema: Pembe na upande ambao walipojitokezea Murji'ah wa kwanza ni utukuzaji wao mkubwa wa Imaan na udunishaji (kufanya duni) wao wa madhambi na ma'asia (yaani; hayo ni mambo yasiyodhuru imani ya mtu) na hudhania yakwamba hilo si jambo la sawa au kuangamia kwa imani ya mtu ni kuzidisha chumvi. Kwahivyo, wao husema: "Hapana dhambi iwezayo kudhuru mahali penye Imani"! Hapo ndipo palipotokea Upotofu wao.

Na kuhusu hawa watu wa leo, basi kipembe chao na upande walioushikilia wao ni katika kuzitukuza siyasa kiasi cha kwamba yoyote aliye pamoja wao katika harakati zao basi huyo atakuwa ni mtu mtiifu. Na ikiwa mtu atakuwa na ufahamu mzuri wa pote lao [malengo yake na makusudio, n.k] basi hakuna dhambi yoyote itakayomdhuru mtu huyo, **hata kama atamshirikisha (Shirk) Mola wa Walimwengu!!!** Kwani wewe huoni jinsi viongozi wao na waandalizi wao wakuu wanavyotumbukia ndani ya mijidhambi

mikubwa, na wao hata hawababaiki kwa fedheha ya aibu (kwa ajili ya dini). Fedheha hii ni kwenye pote lao na vyama vyao!! Kwani wewe huwaoni wanavyogutuka na kubabaika pindi Shaikh 'Abdul-'Aziz bin Baz na Shaikh al-Albani wanaposema yakwamba kwenda katika vita vya umwagaji damu na mayahudi viachiliwe mbali na badala yake uangalifu uzingatiwe katika kuwajenga nguvu zao Waislamu mwanzo [kabla ya kujiingiza vitani ambapo hapana shaka yoyote yakwamba watauwawa]. Na hii ni fatwa kutoka kwa mujtahidoon wa kikweli na kihakika (yaani; wale wenye kustahili kutoa fatwa kuhusu mambo kama hayo).

Hatahivyo, mmojawapo wa viongozi wa mapote hayo anapofanya makosa, basi ni wajibu unaowapasa walio kwenye pote hilo kuangusha macho yao na wala wasitambue yanayoendelea, bila ya kujali matokea yake ya kutisha na kutahayarisha.

Na ni mara ngapi wanapotoa hukmu kuhusu umwagaji wa damu na uporaji wa mali na kisha wakasonga mbele kumwaga damu bure. Lau kama kwa hakika wangelifika daraja ya kuwa wanafunzi wa ki-ilimu, basi hili ndio lingelikuwa jambo bora wangelidhaniwa nalo.

Mchukulie huyu Ali bin Haj (Algeria) kwa mfano, anatoa fatwa ya kuuwawa maelfu ya Waislamu na kufukuzwa wenye kubakia na pia kwa vurumai na tisho katika miji iliyotulia (iliyo na usalama na hali ya utulivu). Na zaidi ya hayo, chochote asemacho katika kusifu na kuitukuza democracy na mambo mengine kama hayo ambayo tuliyoyadondoa kutoka kwake. Sasa pamoja na hayo yote hapana yoyote anaemlaumu, kulingana na maoni yao, isipokuwa ni kibaraka (wa Serkali)!!

Na kabla yake, Sayyid Qutb aliwashutumu na kuwalaumu baadhi ya mitume wa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, na pia kuwakosoa baadhi ya maswahaba walioahidiwa Pepo. Yeye pia alizingatia yakwamba siyasa za Sheriya ya ki-Islamu zimejumuishwa na siyasa za Ujamaa. Kuna mambo mengine mengi yaliyofafanuliwa na Shaikh Rabi' al-Madkhali katika kitabu chake kipya kilichotoka hivi karibuni, na Sheikh al-Albaani alisema kumuhusu yeye (Sheikh Rabee'), "Kwa hakika mshika bendera ya utaalamu wa ukosoaji na utathmini (Jarh-wat-ta'deel) leo, katika zama zetu hizi ni ndugu yetu, Dr. Rabi' na wale wenye kumkosoa yeye hawamkosoi kutokamana na misingi ya ki-Ilimu kabisa, na ilmu kwa hakika iko upande wake…" Kwahivyo hii ni tazkiya ya Sheikh Rabi' kutoka kwa mta'alamu wa ukumbi wenyewe! [8]

Kisha akaja kwenye msururu huu Turabi na madai yake hayo yaitwayo Taifa la ki-Islamu la Sudan na ndie mwenye kupanga mihadhara kwa lengo la kuunganisha Dini zote, na pia kwa min-ajil ya kusifu na kutukuza dini za wenye kuabudu makaburi na pia kwa ajili ya kusimamisha idadi kubwa ya makanisa, ambayo haijawahi kupatikana kabla ya zama zake, hata katika Serikali za wasioamini Mungu. [Na yeye ndiye mwenye kuitisha mchanganyiko wa wake na waume kwenye jamii, na huku akitafuta njia za kuondosha na kuzuiya adhabu zilizofaridhiwa katika Sheriya (hudood)].

Kisha utawakuta (wanaharakati wa kisiyasa) wakiwalegezea kamba wa-Afghani, mpaka utawaona hawabadilishi kitu chochote kutoka katika dini ya wenye kuabudu makaburi na

kufanya ma'asia. Badala yake, wanagombana na watu wa Tauheed kwa kutetea mambo ya Taaghoot (ya hawa wenye kuabudu makaburi n.k)! Na njama zao na uhaini dhidi ya uongozi wa Kunar al-Islaamiyyah ambao hatujausahau katika fahamu zetu!! Na huu ndiwo mji wa pekee katika Afghanistan uliokuwa na msimamo wa Tauheed, na ndipo ambapo swala ziliposimamishwa katika njia inayostahiki pamoja na hudood kutekelezwa. Na hapakuwa na mji wowote uliojulikana katika kupiga vita madawa ya kulevya zaidi ya mji huu. Lakini mara serikali ya Ikhwan-ul-Muslimeen ikaja na kuondoka patupu na hasira nyingi, wakaanza kutangaza vita na watu hawa na hatimae wakamuuwa amir wao, Sheikh wa ki-Salafee, Shaikh Jameel ur-Rahmaan – Mwenyezi Mungu Amrehemu. **Kwahivyo, hapana shaka kuwa wao wamechanganya baina ya madhambi makubwa ya Shirk na kuuwa nafsi bila ya haki yoyote.**

Sasa kuna mambo chungu nzima hayo na mengi zaidi, lakini haina madhara yoyote kwenye Imani yao! Na wala hayo hayasababishi kuupoteza uongozi wao! Lakini badala yake, Ole wake hata yule mwenye kufikiria kuhusu kuwapinga, kwani atakuwa amewatukana wenye kuthibitisha Jihad. Kwa hakika, wao wameyaweka matumaini yao juu zaidi – katika fedheha hizi na mambo ya kuzua yenye kufikia daraja ya kufr – yakwamba ati nchi inayotumainiwa kuwa ya ki-Islamu ya kikweli ni ile ya Afghanistan and Sudan!! Kama ilivyonukuliwa kwenye kanda ya tepu ya Salman al-Awdah, "Ni kwanini wana Khofu na Uislamu". Na kwa hakika huo si ukweli kama alivyosema Allaah, Aliye juu zaidi:

(Kuingia Peponi) si kwa matamanio yenu, wala si kwa matamanio ya watu waliopewa Kitabu (kabla yenu. Lakini mambo ni haya): Atakaefanya ubaya atalipwa kwa (ubaya) huo wala hatapata mlinzi wala msaidizi kwa ajili yake mbele ya Mwenyezi Mungu. [Soorah an-Nisaa – 4:123]

Ni kwa ajili hii ndio baadhi ya wenye Ilmu wamewadhania wao kuwa miongoni mwa Murji'ah washupavu, kwa sababu hawa Murji'ah (wa kawaida) wameiheshimu Iman, na ni katika nguzo za dini. Lakini kuhusu jamaa hawa, basi wao wameiheshimu sehemu miongoni mwa sehemu nyingi za dini, ambazo ni siyasa, ikiandamana na Ilmu walizonazo yakwamba aina ya siyasa zao haitenganishi baina ya siyasa za Ujamaa na Demokrasia. Haya si mageni kwa yoyote aliyewahi kusoma vitabu vya Sayyid Qutb na wengineo mfano wake. Bali, sema kwa ufupi, "Hii ni fiqh ya pote (la kisasa) la uzushi". Murji'ah hawakupinga kuhusu madhara yaliyosababishwa kwa mtu mwenye Imani kwa sababu ya kufanya Shirk, wametambua hayo pamoja na kufr, hakuna wema wowote utakaomfaa. Lakini, kuwahusu hawa [tulio nao leo], basi wao wanawaombea wanavyuoni (hao), hata kama waliyazungumza juu ya kufr iliyo dhahiri na wazi.

La Nne: Suala hili limeandamwa na suala jengine kuhusiana na Murji'ah, nalo ni kutoweka kwao katika kuzifafanua Sunnah kwa watu, na kujiepusha kwao na kuwasuta watu wazushi. Ibn Taymiyyah – Mwenyezi Mungu Amrehemu – Amesema, baada ya kuzungumza kuhusu watu wa takfir:

"Na kwenye nyuso za wale wenye kufanya takfir juu ya upotofu, ni watu wasioielewa 'Aqeedah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah kama inavyostahiki

kujulikana, au wanaijua baadhi yake na ni wajinga kuhusu baadhi nyengine. Hatahivyo, chochote wakijuacho, huwa kawaida hawakielezi kwa watu na badala yake huficha [9]. Na wala hawayakatazi mambo ya uzushi yenye kwenda kinyume na Kitabu na Sunnah[10], wala hawawasuti watu wazushi na wala hawawa-adhibu [11]. Kwa hakika, huwenda hata wakasimama kidete na kupinga mazungumzo ya Sunnah na kanuni za misingi ya dini [yaani; Tawheed n.k] [12]. Au watakuwa tayari kumpokea kila mmoja, wakiwa kwenye madh-hab zao tafauti [13]… Mkuruba huu umewashinda Murji'ah wengi, baadhi ya wana-Sheriya, ma-Soofee, na wanafalsafa (Philosophers). Na mikuruba yote hii miwili (yaani; misimamo ya Takfiri na yale ya Murji'ah na wenye kuwa nao) yako katika upotofu, na nje ya (mipaka ya) Kitabu na Sunnah." [14]

Na wala hutopata watu wawili watakaogombana yakwamba huu ni mmojawapo wa misingi mikubwa ambayo dini ya wanaharakati wa kisiyasa inapozunguka. Na kwani kuna yoyote apingae kanuni zao [zilizo mashuhuri], **"Tupeane udhuru kuhusu yale tunayokhitilafiana na tuungane mikono juu ya yale tunayokubaliana nayo"!!** Na nimeyaeleza hayo katika kurasa zilizotangulia – kutoka katika matamshi ya Hassan al-Bannah – yakwamba kwa hakika wamemaanisha kila aina ya tafauti, yaani, bila ya shaka yoyote! Wameyasema hayo kwa sababu iwapo wataanza kuwapinga na kuwasuta watu wa Uzushi, basi watapoteza wafuasi wao wengi, wale waliozidi katika upotofu.

Lakini hawakomi hapo kwa watu wenye mambo ya kuzua, bali wanaendelea mpaka kwa makafiri. Yameshatangulia katika matamshi ya Ikhwan ul-Muslimeen yakwamba wao wamemakinika kwa kuwa na undugu na Makafiri, kwa hakika hata kuomba mambo hayo kutoka kwa Makafiri, kama nilivyo yanukuu maneno kutoka kwa Hassan al-Bannah na Qardhawi aliyesema yakwamba hakuna utesi kuhusu Dini baina yetu na Mayahudi!! Haya kumebaki nini baada ya hayo?!! [15]

Kwahivyo, hii ni misingi minne ambayo wameafikiana nayo na Murji'ah. Sasa ni nani miongoni mwa watu wanaostahili zaidi kusifiwa na Irja'? Msemo huu si wa kweli kuwahusu wao?!!

Maelezo

[1] Na katika kutoa mifano ya mifumo ya misimamo ya Khawaarij kulingana na maneno ya wanaharakati wa kileo na wenye kuleta mageuzi katika siyasa:

Sayyid Qutb, mashauri mkuu na kiongozi wa Khawaarij-mamboleo, ambae maandishi na vitabu vyake ndio chimbuko na chanzo cha wanaharakati wa siku hizi wa kisiyasa [fee Dhilaal-al-Qur'aan 2/1057], amesema: **"Na mwana-adamu ameikanusha dini (kwa kuelekea) katika ibada ya waja [wa Mwenyezi Mungu] na kuzidhulumu dini. Na wameipa nyongo kalima ya 'Laa ilaaha illallaaha' (shahada) – hata kama kipote kidogo miongoni mwao hubakia kuyakariri matamshi hayo ya 'Laa ilaaha illallaaha' juu ya vinara vya misikiti bila ya kuyazingatia na kuyakusudia maana yake, utamkuta mtu akiyarudia bila ya kukanusha utungaji wa Hakimiyyah ambayo wana-adamu wamjidai kuimiliki."**

Na akaendelea kusema **"Isipokuwa utakuta wanaadamu wamerudi kwenye zama (za mwanzo) za Jaahiliyyah na waka'asi kutoka kwenye 'Laa ilaaha illallaaha', kwa kuwapa wale wana-adamu sifa maalum za Uloohiyyah na kutoithamini Tawheed ya Allaah na hawakuwa ni wenye kunyenyekea kwa utiifu kwake Yeye pekee."**

Kisha akafuatiza hayo na, **"Wana-adamu wote, wakiwemo wale wenye kuyakariri kutoka kwenye vinara vya misikiti, katika sehemu za mashariki na magharibi za Ulimwengu mzima, matamshi ya 'Laa ilaaha illallaaha', bila ya [kuyazingatia] maana yake wala uhakika wake, basi hao ndiwo wenye madhambi makubwa kushinda watu wote na ndiwo watakao adhibiwa zaidi siku ya Kiyama, kwa sababu wao *wameritadi* (wamewacha dini) kwa kuelekea kuwa-abudu waja (wa Mwenyezi Mungu)."!!???**

Huku ni kuchanganyikiwa na ni mambo ya kushangaza kuona yakwamba hawa Qutubiyyah, Surooriyyah, Khawarij-mamboleo, hawagutushwi na ukweli yakwamba kwa kutumia misingi yao wenyewe kutamfanya mshauri wao mkuu na kiongozi, Sayyid Qutb awe ***MURTAD*** (aliye acha dini)!!! Kwani wao hawaoni yakwamba yeye amemkejeli na kumshutumu Kaleem-u-Llaah, Musa (alayhis-Salaam) na pia baadhi ya vipenzi watukufu wa Mwenyezi Mungu. Alimsifu Musa (alayhis-Salaam) kama mtu mwenye **"taharuki"**, mwenye haraka **asiyetuliza fikira zake**, mtu **aliyechachawika** na **mwepesi wa kuhamaki"** (Tasweer al-Fannee uk.154) na akaendelea kusema zaidi, **"Hebu tumuacheni kwenye nukta hii (ya historia) kisha tutamrudia baadae kwenye kikao chengine cha maisha yake, baada ya miaka kumi, ndio pengine atakuwa ameshatulia na kumakinika na nafsi yake"** kisha akaendelea, **"Basi hebu tumuacheni kwa muda ili tujionee jinsi mapito ya nyakati yatakavyomfanya huyu kijana mwenye ghadhabu nyingi"!!!**

Kwani wao hawakuona yakwamba Shaikh Bin Baaz – rahimahullaah – alipoyasikia maneno ya Sayyid Qutb baada ya kusomewa, alisema, **"Istihzai ya Mitume ndiko kuritadi kwenyewe [kutoka nje ya dini]."** [Wakati wa darsa ya Shaikh 'Abdul - 'Azeez ibn Baaz - rahimahullaah – katika nyumba yake huko Riyaadh]. Sasa jee, hawa wachipuzi-wapya wenye fahamu za kijinga wanaodai kwa ubingwa wa ndimi zao, wako tayari kusema yakwamba Sayyid Qutb ameritadi kutokana na matamshi yake hayo??!!

Inataka ifahamike kuanzia sasa, yakwamba wao ndiwo Murji'ah kihakika kwani maafa na mambo ya uzushi mfano wa hayo ya Sayyid Qutb, Mawdudi, Turabi, na wengineo hawaidhuri Imaan kulingana na maoni ya hawa wanaharakati.

Amesema Salman Awdah katika kanda ya tepu, "Jalsah ala ar-Rasif" kuhusu muimbaji mwenye kufanya ufasiki waziwazi, yakwamba, Allaah hatomghufiria madhambi yake! Mpaka atubie, kwa sababu Mtume (sallallaahu alaihi wasallam) alihukumu yakwamba hatosamehewa [akisema] 'Ummah wangu wote utasamehewa'…! **Hii ni kwa sababu wao wameiwacha dini (*murtaddoon*) kutokana na hicho kitendo chao!![*]… Huku ni kuiwacha dini ya ki-Islamu!!** Huyu atakaa motoni milele – na kujilinda ni kwa Mwenyezi Mungu – mpaka atubie!! Kwanini? Hii ni kwa sababu wao hawayaamini maneno ya Mwenyezi Mungu, Mtukufu na Mwenye nguvu, "Wala musiikurubie Zinaa

(kitendo cha uzinifu), kwa hakika (kitendo hicho) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbovu mno" Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona nyote! Yule mwenye kuthibitisha yakwamba kitendo cha zinaa ni haramu na uchafu na (ni kitendo) kinachomuudhi Mwenyezi Mungu. Jee, mtu atakuwa ni mwenye kujivunia (kuhusu dhambi zake) mbele ya watu? Mbele ya halaiki ya watu?!... Haiwezekani mu'min kufanya kitendo hicho!..."

[*] Hii ni manhaj ya Khawaarij, safi na wala isiyokuwa na tashwishi yoyote. Awdah hakujibakishia hata kichochoro cha kuweza kutoroka kwenye mtego huu, kwa jinsi matamshi yake yalivyo wazi, ati watu aina hiyo ni *murtaddoon* kwa ajili ya dhambi tu.

Akasema Aa'id al-Qarnee, katika u.k 335, katika kitabu akiitacho "al-Misk wal-'Anbar', "Na haya – yaani vitu vyenye kulevya – **ndivyo vitu viovu zaidi vyenye kusababisha kumu'asi Mwenyezi Mungu katika ardhi hii!!"??[**]**

[**] Kwani hilo ni kubwa kuliko msiba mkubwa zaidi wa Turabi? Na Serikali ya Sudan, ambayo kulingana na hawa wachipuzi-wapya wenye fahamu za kijinga, ati ni mfano mwema wa Serikali ya ki-Islamu??!! Sasa wataka kusema yakuwa hayo ni makubwa kuliko kufr, shirk, na bid'ah zipatikanazo kwenye hiyo iitwayo Serikali ya ki-Islamu?? Hayo ni makubwa kuliko shirk ya wenye kuabudu makaburi wapatikanao huko Afghanistaan?!

Na Safar al-Hawali akasema katikia mwishoni mwa upande wa kwanza na mwanzoni mwa upande wa pili wa kanda yake ya tepu iitwayo 'Duroos ut-Tahawiyyah (2/272), "Huu mji mkuu ni mfano wa hoteli katika mojawapo ya Miji ya Guba (Gulf states), Dubai… Katika hoteli hii – kuna yule asemae – akitangaza waziwazi – kuna vinywaji katika hoteli hii, waviitavyo vinywaji vya kiroho, ikimaanisha khumoor (aina tafauti za ulevi) huletewa katika yale yapatikanayo ili kuwaburudisha pamoja na video na starehe nyenginezo. Sasa huu ni mwito ulio wazi bila ya tashwishi yoyote – na watu wote walioko hapo hufurahi kwa hayo – na ndani yake hupatikana wenye kuthibitisha yakwamba wao… - na kujilinda ni kwa Mwenyezi Mungu – wamechnaganya kucheza rumba na kuonyesha nyuchi zao pamoja na kunywa khamr (mvinyo). Twajilinda na Mwenyezi Mungu na Ukafiri huu (*kufr*), **kwa sababu hapana shaka yoyote yakwamba kuyafanya yale ambayo yaliyoharamishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa ni halali (istihlaal), ni kufr iliyo wazi pasi na shaka yoyote!!!"**

Mimi nasema: Hebu zingatia kwa makini ndugu yangu! Yeye tayari ameshaifanya hali hii ya utendaji wa madhambi waziwazi kisha akiita sababu, au kilicho sababisha, kuwa "istihlaal". Na kisha akajenga hoja na haraka akarukia hukmu ya takfir, wala hakuwacha nafasi kwenye hukmu hiyo ya kukifasiri kitendo hicho kuwa ni "Kufr-Doona-Kufr" (kufr-ndogo), badala ya kusema, "[Imedhihirika] kuwa ni ukafiri ulio wazi (kufr-saheeh). Na makosa makubwa ya kijinga ya hawa jamaa kuhusu suala la "istihlaal" ndilo lililowachukuwa kwenye malisho ya madh-hab ya Khawaarij. Na lau kama si hivyo, basi kuna tafauti gani baina ya madhambi haya na madhambi mengine. Kwani haiwezekani kumpata aliyefanya dhambi kwenye ulimwengu huu, ambae asiyemkaribisha mshirika

wake au mwenzake katika kufanya ma'asiya? Amma kwa hakika haya ni mambo yenye kutusikitisha kuona yakwamba ni mafundisho ya Aqidatut-Tahawiyyah!

Na twauona mfumo wa Aa'id al-Qarni kuwa hauna tafauti na yale matamshi yake ya awali aliyojitenga nayo kutokamana na baadhi ya makosa makubwa akisema: 'Kumi na nne: nimesema kwenye kanda ya tepu, 'Yoyote mwenye kufanya ni waajib kwa watu yakuwa awe ni Ikhwani au Salafi au Tablighi au Sururi, basi ni lazima atubie. Emma atubie au auliwe.' Mimi nakubali yakuwa haya ni makosa kutoka kwangu na namuomba Mwenyezi Mungu msamaha kutokana na matamshi hayo. **Maana ya matamshi yangu nikwamba yoyote aliyefanya hayo, basi huyo amezua (katika dini).** Hatahivyo, hayo ni makosa kwa hali yoyote, na naomba msamaha na kujiepusha na hayo. Mimi naamini yakwamba madh-hab ya Salaf ndiwo mfumo wa sawa na ndiyo madh-hab iliyo waajib kwa watu kujinasibisha nayo na kuiandama, kuongozwa na kuipitia njia hiyo." [angalia al-Ajwibah al-Mufidah cha Jamal bin Harith].

Sasa al-Qarnee atakuwa tayari kuutumia msingi huu aliwouweka kwa maelfu ikiwa si mamia ya maelfu ya wazalendo waliolazimisha watu wawe Hanafi, au Maliki, au Shafi'i? Na ni nani aliyepasisha yakuwa ni haraam kuchagua kutoka katika kila madh-hab. Jee, atamuhukumu hapa kila mmoja wao kuwa amezua katika dini, na kwahivyo, akawa ametoka katika dini na kuwa *Murtad*? Twamuomba Mwenyezi Mungu ayaangamize haya matamaniwa ya nafsi yasio na kibali chochote na ujinga!!

Ndio Sheikh al-Albaani akaulizwa kuhusu kitabu, "Dhahiratul-Irjaa fil-Fikr al-Islami" cha Safar al-Hawali, na katika kitabu hiki takfir imepitishwa juu ya matendo ya baadhi ya dhambi fulani! Akajibu, "Mimi nilitoa maoni yangu kuhusiana na suala hilo zaidi ya miaka thalathini sasa nilipokuwa nikifundisha katika Chuo Kikuu (cha ki-Islamu) cha Madina na pia nikaulizwa rai yangu kwenye darsa kuhusu Jamaa'at ut-Tabligh. Kwahivyo mimi nikasema siku hiyo, 'Hawa ni Sufi wa zama zetu'. **Na sasa imenidhihirikia mimi yakwamba inanipasa kusema kuhusu pote hili lililojitokeza katika zama zetu hizi na ambao waliowapinga Salaf, hapa mimi nasema, kulingana na matamshi ya al-Hafidh adh-Dhahabi: Wao wamewapinga Salaf katika mas-ala mengi ya manhaj, na inastahiki mimi niwabandike jina la Khawaarij wa zama zetu. Na huu ni msimamo unaofanana na kuchipuka kwao katika wakati huu tulionao – ambapo twasoma kuhusu nakala zao – kwa sababu wao, kwa hakika, maneno yao yanaandama njia na malengo yaleyale ya Khawaarij katika kupitisha hukmu za takfir kwa yule mwenye kufanya madhambi makubwa.** Na pengine ningelisema, haya yametokana na ujinga kwa niaba yao au kwa ajili ya njama iliyobuniwa!! Na nayasema haya kutokana na muangaza wa [maneno ya Mwenyezi Mungu], "Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia insafu (uadilifu). Fanyeni uadilifu; huko ndiko kunakomkaribisha mtu na utawa. [*Soorah al-Maaida 5:8*]. Mimi sijui iwapo wao wanasema yakwamba kila dhambi kubwa ni zenye kumtoa mtu nje ya mkunjo wa Uislamu! Hatahivyo, mara nyingi wao huzunguka kwenye baadhi ya madhambi makubwa lakini hunyamaza au huyapita kimya baadhi nyengine ya madhambi makubwa! Na kwa ajili hii mimi sioni yakwamba tusiwabandike jina hili bila ya masharti au mipaka, na itupasayo kuyasema ni, 'Wao ni Khawaarij', isipokuwa kwenye baadhi ya mas-ala. Na

huu ndiwo uadilifu tulioamriwa kuambatana nao…" [Kanda ya tepu: Surooriyyah ndiwo Khawarij wa zama zetu, mwisho wa upande wa kwanza].

[2] Laalikaa'ee katika Usul ul-I'tiqad [no.1834]

[3]Al-Kitab ul-Latif [no. 17]

[4] Aqidat us-Salaf wa Ashabul-Hadith [109]

[5] Dhahirat ul-Irjaa (1/361)

[6] Imepokewa na Abdullah bin Ahmad katika as-Sunnah (644), al-Khallaal katika as-Sunnah (1230), Ibn al-A'rabi kwenye Mu'jam yake (714), Abul-Qasim al-Baghawi katika al-Ja'diyat (1061), Ibn Battah katika al-Ibanah (1235), al-Lalikaa'ee katika Usul ul-I'tiqad (1841) nayo ni Hassan.

[7] Imepokewa na al-Khallaal katika as-Sunnah (1061), al-Aajurree katika ash-Sharee'ah (u.k 139) na wengineo. Yanayofanana na hayo pia yamepokewa na Ibn Shahin katika 'al-Kitab al-Latif' (16) na al-Lalikaa'ee katika Usul ul-I'tiqad (1835). Kukatika kuliko wazi kwa upokezi katika silisili ya Athar haudhuru chochote kwa vile kuna yaliyofanana nayo yenye muungano wa silisili iliyo saheeh katika Tahdhib ul-Aathar of at-Tabari (1519) na mengine kama hayo pia yametajwa kutoka kwa Sufyan. Angalia katika al-Hilyah cha Abu Nu'aym (7/33) na al-Abaateel cha Jawzjaani (42).

[8] Kanda ya tepu ya "Manhaj al-Muwaazanaat" ya Tasjeelaat at-Tayyibah kutoka Medinah an-Nabawiyyah.

[9] Kama vile walivyo baadhi yao kutoka Ikhwan ul-Muslimeen waliolelewa juu ya Salafiyyah lakini u-hizbiyyah (uzalendo) wao unawazuiya kubainisha na kufafanua 'aqeedah ya Salafi na ambao huwaamrisha kushikamana na mafungamano na madh-hab maalum na pia wenye kuwakataza kuwaonyesha watu mambo ya Sunnah yaliyo kwenye madh-hab nyengine. Hii ni kwa sababu jambo hili litasababisha mgawanyiko baina yao kulingana na fikra zao!

[10] Yapitie maneno ya Hassan al-Bannah katika Mudhakkiraat ad-Da'wah wad-Daa'iyah (u.k 64-65) kuhusu dharura za kunyamaza kuhusu ikhtilafu zijulikanazo katika mas-ala ya 'aqeedah kama vile kujumuisha mafunzo ya ki-Sufi, kufanya tawassul kwa kupitia watu wema, na kuomba du'ah kwa kupitia waliokufa! Na mwisho akasema, "Na Waislamu wamehitilafiana kuhusu mas-ala haya kwa mamia ya miaka, na hawatowacha kukhalifiana. Na Mwenyezi Mungu, Mtukufu Aliye juu anapendezwa na mapenzi (miongoni mwetu) na umoja.!!"

[11] Kama walivyo Ikhwan wasemao, "Sisi twapinga mambo ya uzushi, lakini hatumlaumu mwenye kufanya (mambo ya uzushi) au muanzilishi! Na hatuyapendi mambo hayo ya uzushi, lakini hatumchukii mwenye kufanya (mambo ya uzushi)!!!"

[12] Kama walivyo Ikhwan wasemao, "Kuzungumza kuhusu Sunnah ni jambo dogo lisilo na maana. Na kuzungumza kuhusu Majina ya Mwenyezi Mungu na Sifa Zake [si chochote zaidi ya] falsafa na ni upotezaji wa wakati."!!

[13] Kama walivyo Ikhwaan, kwani "Utadhani kuwa wameshikamana pamoja, lakini nyoyo zao zimetawanyika, na ziko mbalimbali" kwani miongoni mwao kuna Sufi na tariqa zao zote, Ash-'aree, Maatureedi, Raafidha, Jahmi, na Mu'tazilah.

[14] Majmu' ul-Fatawa (16/427) pia angalia Bada'i ut-Tafsir cha Ibn al-Qayyim (5/548)

[15] Amma kuhusu Ikhwan ul-Mufliseen, basi wao wamesema katika al-mujtama' (tarehe 30th Dhil Qa'dah 1415), **"Msimamo wetu kuwahusu ndugu zetu, makristo wa Egypt na Ulimwengu wa Waarabu ni maarufu sana na wa zamani na ulio wazi na wa kipekee: Yanayowapasa wao ndiyo yanayotupasa sisi, na makubaliano yao ndiyo makubaliano yetu. Wao ni washirika wetu katika nchi hii. Katika mapambano yetu marefu ya harakati kwenye nchi hii, wao ni ndugu zetu na kila haki ya nchi inawapasa wao, ki-Uchumi na kiroho, ki-Dini na ki-Siyasa… na yoyote mwenye kusema chochote kinyume cha haya basi sisi tuko mbali nae na yote ayasemayo"!!!**

Na pia wakabuni kamati ya Shura ya ki-Islamu kama ndugu katika Demokrasia ya ma-Kuffaar, wakisema**: Na iwapo Shura ina maana yake maalum ya kipekee katika mtizamo wa ki-Islamu, basi katika asli yake ni sawa na hukmu za Demokrasia (nidham al-demoqratee)".**

Na hili azimio lao pia lina maombi kwa Serikali la kufuata mapatano chini ya Sheriya zisizokuwa za dini, sio Shari'ah (ya ki-Islamu). Wakasema, **"Ili Ikhwaan iendelee kudumu, imenyenyekea kwa Serikali yakwamba wasikabiliane nao kwa ukali, na badala yake wawe ni wanyenyekevu juu ya kanuni za hukmu za ki-Serikali na amri zake. (akham al-qanoon wal-qadaa)."**

Bali, wao wenyewe wameridhika na kutosheka na hayo kama walivyoendelea kusema, **"Hatahivyo, wao (Ikhwaan), wameendelea na kuzidi kudumisha utiifu wao juu ya nidhamu za ki-sheriya na katiba ya nchi (ahkam ad-dustoor wal-qanoon)…."**

Na wala hawakusema haya kwa taqiyyah (udanganyifu), lakini (wameyasema) juu ya kutosheka, kama vile wao wenyewe walivyojishuhudilia nafsi zao, wakazidi kusema, **"Na suala nyeti (lenye uzani) katika haya yote, si ya kisiyasa wala utumiaji hila, lakini ni suala la ki-Dini na 'Aqeedah (din wa aqidah), na juu ya yale ambayo Ikhwaan watakayokutana na Mola wao, "Siku ambayo mali na watoto hayatomfaa mtu. Isipokuwa kwa yule atakaekuja na moyo uliosalimika na uliotakasika."**

Na kisha kuna maneno ya Hassan al-Bannah, **"Na mimi nathibitisha hapa yakwamba ugomvi wetu na Mayahudi hayahusu mas-ala ya Dini kwa sababu Qur'aan imetuhimiza sisi tufanye usuhuba na wao na tuwapokee kwa vizuri. Na Uislamu ni**

Shari'ah kwa Wana-adamu wote kabla ya kuwa ni Sheri'ah kwa pote la watu maalum. Na (Uislamu) umewasifu wao (Mayahudi) na ukaweka makubaliano baina yetu sisi na wao, "Na msibishane na watu waliopewa kitabu (kabla yenu) ila kwa yale (majadiliano) yaliyo mazuri". [Soorah al-'Ankaboot 29:46] **Na pindi Qur'aan Tukufu inapotaja mas-ala ya kuhusu Mayahudi huingilia kwa njia ya ki-Uchumi na maoni ya ki-Sheriya…"!!!** [Ikhwan ul-Musilmoon, Ahdaath Sana'at Tarikh (1/409-410)]

Na Qardhaawi nae akasema, katika kuongezea maovu yaliyopita kiasi ya al-Bannah, **"Vita vyetu na Mayahudi si kwa ajili ya 'Aqeedah (yaani; Dini)!! Sisi twapigana nao kwa ajili ya Ardhi!! Hatupigani nao ati kwa sababu ni ma-Kuffaar!! Twapigana nao kwa sababu wamevamia Ardhi yetu na wameiteka bila ya haki ipasayo"** [Ar-Raayah, 4696 Wednesday, 24th Sha'ban 1415]